

UCHIPUZI WA KILEKSIKA KATIKA MASHAIRI YA SHAABAN ROBERT

Mwenda Mbatiah

Ikisiri

Shaaban Robert ni miongoni mwa waandishi wenye hadhi ya juu katika fasihi ya Kiswahili kutokana na ukubwa na upevu wa mchango wake katika fasihi hiyo. Kuna tahakiki nyingi zikiwemo vitabu, tasnifu na makala ambazo zimeandikwa juu ya tungo zake. Hata hivyo, hatuwezi kusema kwamba uchunguzi juu ya kazi za kigogo huyo umetosha. Bado wahakiki wana kazi kubwa mbele yao. Shaaban Robert aliasisi na kuendeleza tanzu kama vile riwaya, wasifu, tawasifu na insha. Lakini ni katika ushairi ambapo alitoa mchango mkubwa zaidi. Tahakiki nyingi juu ya mashairi yake zinashughulikia maudhui zaidi kuliko fani. Mathalan: A. G. Gibbe (1980), E. K. Kezilahabi (1976) na F. E. M. K. Senkoro (1988). Hatusemi kwamba kuna ubaya wowote wa tahakiki kuelemea kwenye maudhui. Hata hivyo, kuna mengi sana katika fani ya mashairi ya Shaaban Robert ambayo yanastahili kushughulikiwa. Hivyo, mchango wa makala hii katika kuziba pengo hilo ni kuchunguza kipengele kimoja tu katika mtindo wa mashairi ya Shaaban Robert, yaani msamiati, na haswa jinsi mshairi anavyoepukana na ukawaida kutokana na ustadi wake wa kutumia lugha teule. Tunaitathmini leksisi hiyo kwa kuchunguza sababu za uteuzi na umuhimu wake wa kimaana. Kwa ujumla, mwelekeo wa makala ni wa elimumitindo.

Utangulizi

Kama kichwa cha makala kinavyoonesha, huu ni uchanganuzi wa leksisi katika mashairi ya Shaaban Robert. Leksisi ni istilahi ya kiisimu inayorejelea msamiati uliotumika katika matini maalumu (Baldick, 2008; TUKI, 1990). Dhana hii haina tofauti kubwa na ile ya lughateule inayotumiwa katika uhakiki wa kifasihi. Kwa hivyo, kinachochunguzwa hapa ni maneno ambayo mshairi ameteua na kutumia katika tungo zake. Hiki ni kipengele kimojawapo katika mtindo wa mashairi ya Shaaban Robert. Dhana ya mtindo imeelezwa kwa njia mbalimbali na wataalamu tofauti tofauti, na ni telezi mno. Mifano ya wataalamu hao ni kama Enkvist (1964), Crystal & Davy (1969), Hough, (1969), Mwansoko (1991), Verdonk (2002) na wengine wengi. Leech & Short (1981) wanajaribu kuepuka utata na utelezi wa dhana tunayoizungumzia kwa kuiangalia kama matumizi ya lugha katika matini maalumu. Hii ndiyo fahiwa ya mtindo tunayotumia katika

makala hii. Uchunguzi wa mtindo katika viwango mbalimbali kama fonolojia, mofolojia, sintaksia, leksisi, n.k. ndiyo kiini cha taaluma ya elimumitindo.

Kwa mujibu wa Leech na Short (keshatajwa), elimumitindo katika fasihi huwa na lengo la kuelezea uhusiano kati ya lugha ya kazi fulani na uamilifu wake wa kisanaa. Hii ni kusema kwamba tunapoichunguza lugha hiyo, tunajaribu kujibu swali la athari ambayo lugha hiyo inazua kwa msomaji. Athari hiyo ndiyo “uamilifu wa kisanaa” unaozungumziwa hapa, na inahusiana na maana ambayo matini inayohusika inawasilisha. Maelezo ya Simpson (2004) yanaoana na hayo yaliyorejelewa hapo juu anaposema kuwa elimumitindo inahusu kutalii ubunifu katika matumizi ya lugha, na kwamba mtalaa kama huo unarutubisha uelewa wetu wa lugha na pia matini ya kifasihi.

Ni muhimu ieleweke kwamba japo Mwansoko (keshatajwa) anaelezea elimumitindo kama taaluma inayohusu mitindo yote ya lugha katika mawasiliano, mtindo unaotuhusu ni ule wa fasihi. Jambo jingine muhimu ambalo Mwansoko (keshatajwa) anagusia ni kwamba elimumitindo hutumia zana za kiisimu. Maana yake ni kwamba taaluma hii hutumia dhana, istilahi na taratibu za uchanganuzi ambazo zinatumiwa katika isimu. Umuhimu wa taratibu za kiisimu pia umetiliwa mkazo na Ngara (1982) ambapo anafafanua kwamba sifa hiyo ndiyo inayotofautisha uhakiki wa kimtindo na ule wa kikaida ambao unarejelewa kama “uhakiki wa kifasihi”.

Kichwa cha makala hii kimetumia istilahi ya “uchipuzi” ambayo pia inahitaji kufafanuliwa. Tafsiri ya Kiingereza ya istilahi hii na nyingine ambazo zimetumiwa inapatikana kwenye kiambatisho mwishoni mwa makala. Hatua hii imechukuliwa ili kuondoa uwezekano wa suitafahamu kuhusiana na matumizi ya istilahi za Kiswahili. Istilahi ya “uchipuzi” imeundwa kutokana na kitenzi “chipua” ambacho kina maana ya kutokeza kwa mmea mchanga kutoka ardhini baada ya mbegu kupandwa. Katika muktadha wa elimumitindo, kujitokeza kunakorejelewa ni kule kwa matumizi ya lugha. Uchipuzi unahusu kujitofautisha kwa matumizi ya lugha katika fasihi na yale ya kikawaida. Kujitofautisha huko kunayafanya matumizi ya lugha yanayohusika kujitokeza na kuweza kutambuliwa na msomaji kwa urahisi. Aghalabu, uchipuzi unatokana na uvunjaji au ukiukaji kimakusudi wa kanuni za matumizi ya lugha. Tukumbuke

kwamba mwandishi ana idhini ya kishairi inayomwezesha kutumia lugha kwa njia ambayo ni kinyume na kanuni za kisarufi na nyinginezo zinazotawala matumizi ya lugha. Mwandishi anaweza kuvunja kanuni na kaida za lugha katika viwango mbalimbali. Ikumbukwe kwamba waandishi hufanya hivi ili kutilia mkazo jambo fulani au kuzua athari mahususi.

Changamoto mojawapo ambayo mhakiki wa kimtindo anakumbana nayo inahusu ugumu wa kupambanua waziwazi matumizi ya lugha ambayo ni ya kikaida, kwa upande mmoja, na yale ambayo ni kinyume chake, na hivyo yanayoakisi ukengeukaji/ukiushi unaoleta uchupuzi, kwa upande mwingine. Hata hivyo tunaweza kutumia sarufi ya lugha, msamiati wake, otografia, fonolojia na mofolojia kama viwakilishi vya kaida. Yaani, matumizi ya lugha yanayozingatia sarufi, msamiati, sauti na unyambilishaji unaokubalika ndiyo ya kikaida. Matumizi yanayokiuka hata kiwango kimojawapo yanawakilisha uchipuzi. Uchipuzi huo unaweza kufafanuliwa kwa kurejelea kiwango cha kiisimu kinachohusika.

Hata hivyo, uchipuzi unaweza kutokana na matumizi ya lugha ambayo hayahusu uvunjaji wa moja kwa moja wa kanuni na kaida za lugha. Unaweza, kwa mfano, kutokana na urudiaji wa kipashio fulani au upangaji wa vipashio kama vile maneno, sentensi, n.k. kwa njia maalumu. Vyovyote vile ambavyo mwandishi anazua uchipuzi, jambo muhimu la kutilia maanani ni kwamba hufanya hivyo ili kuzua athari fulani inayohusiana na wazo analoniua kuliwasilisha. Kwa vile kipengele cha mtindo tunachokishughulikia ni leksisi, yaani maneno ambayo Shaaban Robert ameyatumia kwa njia ya uchipuzi, inahalisi tueleze kwa ufupi aina za ukiushi unaohusiana na uteuzi wa maneno:

- (a) Maneno ya kizamani: Haya ni maneno ambayo hayatumiki tena katika Kiswahili Sanifu. Washairi huyafufua kimakusudi na kuyatumia kwa sababu mbalimbali kama tutakavyoona.
- (b) Kuchanganya msimbo: Matumizi ya maneno ya lugha za kigeni kama yalivyo katika lugha hizo, bila kuyatohoa.
- (c) Ukopaji: Kuchukua maneno ya lugha za kigeni na kuyatohoa ili yaoane na muundo na sauti za lugha ya Kiswahili.
- (d) Urudiaji: Kutumia neno lile lile mara nyingi, na haswa kwa karibu, kwa njia isiyo ya kawaida.

- (e) Unyambulishaji: Upachikaji wa viambishi kwenye mizizi bila kufuata taratibu zinazokubalika, na kuzua vinyambuo visivyo vya kawaida.
- (f) Nahau: Mfuatano wa maneno mawili au zaidi ambayo maana yake haitokani na maana za maneno ambajengo (tafsiri yangu ya Leech & Short, keshatajwa).
- (g) Kutumia neno kwa njia isiyo ya kawaida kwa kupanua maana yake, au hata kubuni neno jipya.
- (h) Ubadilishaji wa neno katika kiwango cha fonolojia kwa kulifupisha (inkisari), kulirefusha (mazida), au kugeuza sauti zake (tabdila).
- (i) Rejesta: Wingi wa maneno ya rejesta maalumu, na pia matumizi ya maneno kutoka rejesta tofauti tofauti, au kuchanganya rejesta.
- (j) Uunganishaji wa maneno mawili au zaidi
- (k) Matumizi ya istilahi na maneno mengine yasiyo ya kawaida
- (l) Tafida: Matumizi ya maneno mbadala yanayopunguza ukali wa neno linalowasilisha moja kwa moja maana iliyodhamiriwa. Kwa mfano, “aga dunia” badala ya “kufa.”

Orodha hii ni kama mwongozo tu, na siyo lazima aina zote za ukengeukaji wa kileksika zijitokeze katika mashairi yanayohusika. Wala siyo lazima mpangilio wake ufuatwe. Aidha, hii siyo njia pekee ya kufanya uchanganuzi wa kileksika. Njia nyingine inaweza kujikita katika uchunguzi wa kategoria za maneno kama vile vitenzi, nomino, vivumishi, n.k. na ufafanuzi wa sifa zinazohusiana na matumizi ya maneno kutoka kila kategoria (taz. Leech & Short, keshatajwa). Hatimaye, hakuna uchunguzi wa kimtindo wa matini ya kifasihi unaoweza kuelezea kila kitu. Hata mchunguzi anapojifunga katika kipengele kimoja cha mtindo kama leksisi, ni muhali kuweza kutoa tahakiki ya makataa.

Jambo jingine muhimu katika elimumitindo ni kuhusiana na uteuzi wa data. Je, ni kiasi gani cha data ambacho mchunguzi anafaa kushughulikia? Ni sehemu ya kazi ya kifasihi, kazi nzima, au (kwa mwandishi kama Shaaban Robert) tungo zote za mwandishi? Hili ni swali gumu, na kila mchunguzi hulijibu kwa njia yake kutegemea lengo lake. Katika makala hii, tulitumia data ya mashairi ya Shaaban Robert yanayopatikana katika diwani zake takribani darizeni moja.

Hili ni jaribio la kudhihirisha uchipuzi wa kileksika unaotawala katika mashairi yake pamoja na kufafanua umuhimu wa uchipuzi huo.

Uchanganuzi wa data

Baada ya kushughulikia masuala ya kijumla katika sehemu ya utangulizi, tunageukia uchanganuzi wa data ili kubainisha jinsi uchipuzi unavyotokana na uteuzi wa msamiati katika mashairi ya Shaaban Robert. Kote katika makala, maneno yanayoshughulikiwa yamepigwiwa mstari kama njia ya kuyatambulisha.

Rejesta ya kidini

Rejesta ya kidini, haswa dini ya Kiislamu inajitokeza katika baadhi ya mashairi ambayo yametumia mtindo wa dua. Katika tungo za aina hii, msemaji au pasona anamwomba mtu au jambo fulani. Kwa mfano, katika diwani ya *Almasi za Afrika* (uk. 56), tunapata shairi la ubeti mmoja lenye kichwa cha kisitiari: “Dua Dawa”. Msemaji katika shairi anamwomba rafiki yake aitwaye Bwana Rivington, awe na afya, maisha marefu na hatimaye aingie peponi. Kuna maneno kadhaa ya rejesta inayohusika kama vile: dua, Allah, Manani na Peponi. Maneno haya yametumiwa kimakusudi kuitambulisha dini inayohusika na kufanikisha ombi ambalo msemaji anatoa kwa Mungu.

Katika diwani hiyo hiyo, tunapata mfano mwingine ambapo tofauti na huo wa kwanza wa shairi zima ambalo ni dua, huu wa pili ni wa shairi ambalo sehemu yake ni dua. Shairi lenyewe ni utenzi wenye beti 76 na kichwa cha: “Neema Nyingi Ajabu” (uk. 42-52). Sehemu ambayo ni dua inanzia ubeti wa 67 hadi 70. Hapa tunapata maneno mengi ya rejesta inayohusika ambayo yametumiwa kwa njia na sababu iliyotajwa hapo juu. Mbali na maneno kama yale yanayopatikana katika shairi la “Dua Dawa”, hili la pili pia limetumia haya yafuatayo: Tuombe, sali, shetani, Kahari.

Katika mifano miwili ya mashairi iliyotajwa hapo juu, tunaona kwamba neno ambalo limerudiwa zaidi ni nomino ambayo inawakilisha majina mbalimbali ya Mungu katika Uislamu. Majina haya yanajitokeza kwa wingi sana katika mashairi mbalimbali. Kwa mfano:

<u>Jina la Mungu</u>	<u>Kichwa cha shairi</u>	<u>Kitabu</u>	<u>Mahali</u>
Ghafuri	“Siku ya kusafiri”	<i>Pambo la lugha</i>	Uk. 29, ub. 1
Wahabu	“Kwa fulani”	“ “	Uk. 16, ub. 5
Muombwa	“Muombwa”	<i>Mashairi ya Shaaban Robert</i>	Uk. 18, ub. 1
Muumba	“Jua”	“ “	Uk. 7, mst. 5
Bwana	“Mungu”	“ “	Uk. 9, mst. 8
Mwenyezi	“Allah”	“ “	Uk.7, mst. 8
Karimu	“Gossage 1949”	“ “	Uk. 14, ub. 4
Rabi	“Takirima”	“ “	Uk. 5, ub. 1
Jabari	“Barua ya shukrani”	<i>Almasi za Afrika</i>	Uk. 69, ub. 4
Mweza	“Ua langu”	“ “	Uk. 15, ub. 4
Subuhana	“Sijafahamu”	“ “	Uk. 23, ub. 1
Jalia	“Neema nyingi ajabu”	“ “	Uk. 42, ub. 5
Latifa	“Kuzaliwa kwa Mahatma Gandhi Oktoba 2”	“ “	Uk. 29, ub. 1
Mfariji	“Uokovu”	<i>Kielezo cha Fasili</i>	Uk. 30, ub. 1
Wadudi	“Ukaidi”	“ “	Uk. 18, ub. 3
Raisi wa Maseyidi	“ “	“ “	Uk. 19, ub. 14

Jina “Mungu” lenyewe limerudiwa mara nyingi kuliko hayo yaliyotajwa hapo juu. Kwa mfano, katika shairi la “Mbegu za Mungu”: *Mashairi ya Shaaban Robert* (uk. 19-20) limerudiwa katika beti zote kumi. Data hii inaonesha mambo mawili yanayohusiana na ambayo ni muhimu sana katika mashairi ya Shaaban Robert. Kwanza, rejesta ya dini ya Kiisalmu ndiyo inayotawala katika tungo zinazohusika. Pili, rejesta hiyo na haswa majina ya Mungu inaonesha umuhimu wa Mungu katika maisha ya binadamu. Baada ya kuumba mwanadamu, Mungu ameendelea kuyadhibiti maisha yake. Kila jina la Mungu linabeba sifa yake mojawapo ambayo aghalabu inarejelea uhusiano wake na binadamu pamoja na viumbe wengine. Kwa mfano, Manani linaashiria sifa ya Mungu ya upaji; Ghafuri linaashiria sifa ya kughofiri, yaani kusamehe dhambi; Wadudi linaashiria sifa ya Mungu ya kupendwa na viumbe wote; Jabari linaashiria sifa ya

Mungu ya kuwa mtawala mwenye uwezo, n.k. Majina mengine kama Mfariji, Mweza, Raisi wa Maseyidi, n.k. ni sitiari ambazo mshairi amebuni kumsifia Mungu.

Rejesta ya siasa na vita

Japo kwa ujumla, rejesta ya kidini inatawala katika mashairi ya Shaaban Robert, zipo aina nyingine za rejesta ambazo zinaweza kutambulika, na ambazo zina umuhimu wa kimaana katika mashairi yanayohusika. Kwa mfano, kuna rejesta ya kisiasa ambayo inajitokeza katika tungo kama “Istaklali ya Tanganyika” katika *Almasi za Afrika* (uk. 57-58). Neno la kwanza katika kichwa cha shairi ndilo linalojitokeza zaidi kwa sababu ni adimu sana. Linatokana na utohozi wa neno la Kituruki *istiklal* ambalo linamaanisha uhuru. Kama kichwa hiki kinavyodokezea, maudhui ya shairi ni thamani ya uhuru wa kisiasa. Maneno mengine ambayo yametumiwa kuwasilisha maudhui hayo ni kama vile: nchi, utumwa, sheria, bendera, taifa, kutawaliwa na madaraka ambalo mshairi ametumia mbinu ya inkisari kulifupisha ili kupata urari wa mizani. Katika shairi limeandikwa kama “daraka”. Pia, Nyerere amerejelewa katika mstari wa mwisho na kuombewa maisha marefu. Kutajwa kwa kiongozi huyo ni muhimu kwa kuwa ndiye aliyeongoza harakati za ukombozi na kuleta uhuru nchini Tanzania. Matumizi ya rejesta ya kisiasa yamemwezesha mtunzi kuchangia katika ukombozi wa nchi yake kwa kuwafunza wananchi wenzake umuhimu wa uhuru na kwa nini Tanganyika ilistahili kuupata.

Tumejumuisha siasa na vita katika sehemu hii kwa sababu ni mambo yanayohusiana. Vita hutokea mara nyingi kwa sababu za kisiasa, na mataifa hupigana ili kulinda masilahi ya kisiasa pamoja na mengine. Rejesta za siasa na vita zinatawala katika kazi moja ya Shaaban Robert ambayo ni *Utenzi wa Vita vya Uhuru: 1939 hata 1945*. Kazi hii ambayo ni utenzi wa beti elfu tatu, ndiyo ndefu zaidi ambayo Shaaban Robert aliwahi kuandika. Istilahi za kivita zinaweza kuainishwa katika makundi manne kama ifuatavyo:

- (a) Maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza: Sabmarini, parachuti, manowari, bomu, admeri, eropleni.
- (b) Maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kiarabu: Fataki, amiri, shujaa, zana, jeraha, silaha, adui, merikebu, damu, handaki, amri.

- (c) Maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kituruki: Askari, baruti, bunduki.
- (d) Maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kireno: bastola.
- (e) Maneno yanayoelekea kuwa yenye asili ya Kibantu: Kondo, kupigana, shambulia, mzinga, kombora, matopito, mateka.

Pia, kuna neno mwanahewa ambalo linatokana na uunganishaji wa maneno mawili yenye asili tofauti. Nayo ni mwana lenye asili ya Kibantu, na hewa lenye asili ya Kiarabu. Huu ni utaratibu uliozoeleka wa kuunda istilahi za Kiswahili. Data hii inaonesha wingi wa maneno mkopo, hasa kutoka Kiarabu na Kiingereza. Hizi ndizo lugha ambazo zimekuwa na athari kubwa zaidi katika Kiswahili kwa sababu za kihistoria ambazo zinafahamika vyema. Wingi wa maneno yenye asili ya kigeni katika matini inayozungumziwa unaakisi uhalisi wa kwamba suala ambalo matini hiyo inalishughulikia ni la kigeni. Japokuwa historia inaonesha kwamba Waafrika walishiriki (kwa kiasi kidogo) katika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, vilikuwa vita baina ya mataifa kutoka mabara ya nje ya Afrika. Mataifa hayo ni kutoka Ulaya, mathalan Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Italia, n.k. Kutoka Asia, mataifa kama Urusi, Uchina na Ujapani pia yalikusika. Kutoka Amerika Kaskazini, Marekani na Kanada yalishiriki. Ndiyo sababu katika kazi inayozungumziwa, kuna urejelezi mwingi wa mataifa hayo pamoja na viongozi wao. Kwa upande mwingine, kuna urejelezi mdogo kwenye mataifa ya Kiafrika. Ni jambo la kawaida kwamba mtumiaji wa lugha kama Kiswahili anapozungumzia tajriba ambayo ni ya nje ya utamaduni wake, hulazimika kutafuta dhana na istilahi za kigeni ili aweze kuielezea mada yake. Ndivyo alivyofanya Shaaban Robert mintarafu ya dhana na istilahi za kivita zilizotajwa hapo juu.

Maneno ya kizamani

Abedi (1954:34) anaeleza kwamba matumizi ya maneno ya kizamani humsaidia mshairi kuweza kupata idadi ya mizani inayofaa. Kwa kutilia maanani kwamba mtaalamu huyo pia alikuwa mshairi mtajika, maelezo yake ni ushahidi wa kwamba mbinu inayozungumziwa imekuwapo katika ushairi wa Kiswahili tangu jadi. Kufuatana na maelezo ya Abedi (keshatajwa), tunaona kwamba aghalabu, Shaaban Robert anapotumia maneno ya kizamani, huwa ni kwa sababu

iliyotajwa hapo juu. Tunapata mifano ifuatayo kutoka diwani ya *Almasi za Afrika*, shairi lenye kichwa: “Sheikh Ali” (uk. 20-21):

<u>Neno la kizamani</u>	<u>Mahali</u>	<u>Neno la kisasa</u>
1. iondokile	ub. 2, mst. 3	imeondoka
2. waole	ub. 3, mst. 2	watazame
3. itupotele	ub. 7, mst. 3	imetupotea
4. inishikile	ub. 8, mst. 1	imenishika
5. kinibanangile	ub. 9, mst. 1	kinanibananga
6. nipotele	ub. 10, mst. 1	nimepoteza

Katika mifano 2, 3, 5, na 6 ni wazi kwamba maneno ya kisasa ni marefu kuliko yale ya kizamani. Kwa hivyo, kutumiwa kwake ili kupata idadi sawa ya mizani katika mistari ya shairi inayohusika kuna mantiki. Lakini katika nambari 1 na 4, urefu wa maneno ya kizamani na yale ya kisasa ni sawa tukitumia kigezo cha idadi ya silabi. Kwa hivyo, sababu ya matumizi ya maneno hayo siyo urari wa mizani. Sababu ya kutumiwa kwake ni kupata kina cha – **le**, ambacho ndicho kina cha ukwapi, yaani kipande cha kwanza, cha mistari unaohusika.

Kuna sababu ya tatu inayohusiana moja kwa moja na maana au ujumbe wa shairi, na ambayo ni muhimu zaidi. Shairi linalohusika ni la aina inayojulikana kama mbolezi. Hili ni shairi ambalo huomboleza kifo cha jamaa, rafiki au mtu mashuhuri. Katika shairi la “Sheikh Ali”, mshairi anaomboleza kifo cha mtu anayetajwa katika kichwa cha shairi. Mshairi anamwelezea marehemu kama mtu aliyekuwa na hadhi ya juu sana katika jamii ya Tanga. Kifo chake kinawakilisha kupita kwa enzi iliyojaa neema na matumaini. Enzi hiyo ya nyuma ambayo maendeleo yake yaliwakilishwa na marehemu, inarejelewa kwa kutumia maneno ya kizamani. Njia hii ya kuirejelea enzi hiyo inaafiki vizuri, na inatilia uzito ujumbe na umuhimu wa Sheikh Ali na kutowezekana kupatikana kwa mwingine kama yeye. Uzuri wa enzi anayowakilisha na kupotea kwake unasisitizwa katika ubeti wa saba unaosema:

Hairudi Tanga ile, Tanga ya wenye adili,
Walikuwa wapole, kwa fikira na feli,
Zamani itupotele, tuna Tanga ya kivuli.
.... (uk. 21)

Urudiaji

Kuna aina mbalimbali za urudiaji kama vile:

(a) Anafora

Hii ni mbinu ya utunzi inayotumia urudiaji wa neno mwanzoni mwa vishazi, sentensi au mistari inayofuatana. Mbinu hii hutumiwa kuleta msisitizo na pia kuzua ridhimu – yaani ruwaza ya kupendeza kutokana na marudio ya mapigo maalumu. Mfano mmoja ni shairi la “Hofu” katika *Almasi za Afrika* (uk. 32-34) ambapo mistari wa kwanza katika beti zote 21 unaanza na neno “hofu”. Aidha, katika beti kadhaa, mistari inayofuatana inaanza na neno hilo. Kwa mfano, beti mbili za kwanza zinasema:

- | | |
|--|---|
| (1) Hofu zetu ni fitina, wajibu kutahadhari,
Hofu mkiandamana, heri kugeuka shari,
Hofu kufanya mchana, usiku wenye hatari,
Tusizipe mashauri, japo hofu sote tuna. | (2) Hofu japo wote tuna, wasia kitu kizuri,
Hofu kudai hatuna, si neno la ikirari,
Hofu kila mtu ana, aibu ni kukithiri,
Tusizipe mashauri, japo hofu sote tuna. |
|--|---|

Hapa tunapata msisitizo mkubwa juu ya maudhui ya hofu, ikiwa ni pamoja na madhara ya kutawaliwa na hofu, na njia mbalimbali za kukabiliana nayo. Pia, tunapata wazo la kuwa ni maumbile ya binadamu kuwa na hofu, lakini tunapaswa kuidhibiti. Mfano mwingine wa urudiaji wa kianafora ni katika shairi la “Kweli” linalopatikana katika diwani ya *Masomo yenye adili* (uk. 5-11). Mistari ya kwanza ya karibu beti zote 25 inaanza na neno “kweli”. Aidha, kama ilivyo katika shairi la “Hofu”, kuna beti kadhaa ambapo mistari inayofuatana inaanza na neno linalohusika. Kwa mfano, ubeti wa tano unasema:

Kweli nuruye hekima, mwenye nayo ana haki,
Kweli haifichi nyuma, la haramu na mutlaki,
Kweli ukiwa mzima, fanya nayo itifaki,
Ni kitu kwetu lazima, kwa heba na urafiki.

Kama ubeti huu unavyodokezea, mbinu ya anafora imetumiwa kutilia mkazo umuhimu mkubwa wa ukweli katika maisha ya binadamu. Kwa sababu mashairi mengi ya Shaaban Robert huwa yamedhamiriwa kuwasilisha mafunzo yanayohusiana na maadili, mashairi hutumia njia mbalimbali kuleta msisitizo kwenye maadili anayofunza. Anafora ni mbinu ambayo ameitumia kwa wingi.

(b) Epanalepsia

Hii ni mbinu ya urudiaji ambapo neno linatumiwa, kisha linarudiwa baada ya kukatizwa na maneno mengine. Kama anafora, mbinu hii pia hutumiwa kuleta msisitizo. Kwa mfano:

Ua hili kama kito, ua hili kufu yangu,
Ni ua kweli si ndoto, ua ni kipenzi changu,
Ni ua lenye mnato, limevuta moyo wangu,
.... (taz. “Ua” katika *Kielezo cha Fasili*, uk. 35, ub. 2)

Neno linalohusika limepigwa mstari. Mbali na kuleta msisitizo kwenye mada ambayo shairi zima linazungumzia, urudiaji wa neno “ua” unawasilisha hisia ya kimapenzi iliyomtawala msemaji anapozungumza juu ya mpenzi wake anayewakilishwa na sitiari ya ua. Hii ni sitiari inayoashiria uzuri wake, mithili ya ule wa ua halisi, na jinsi anavyomvutia msemaji. Japo mbinu tunayoizungumzia haijatumiwa kwa wingi kama anafora, inazua athari kubwa kila inapojitokeza.

(c) Kibwagizo/kituo

Huu ni mstari ambao unarudiwa mwishoni mwa kila ubeti wa shairi. Kuwapo kwa kibwagizo au kituo ni nguzo mojawapo ya ushairi jadi wa Kiswahili. Abedi (keshatajwa) anaelezea kanuni zake kwa kusema: "*Desturi iliyoenea zaidi ni kukifanya kituo kuwa kiini cha habari, na kukileta mwisho wa kila ubeti bila kubadilisha maneno yake.*" Japo baadaye katika ufafanuzi wake anaeleza kwamba kibwagizo huweza kubadilisha maneno yake kwa kiasi kidogo, kaida inayotawala ni ile ya kuwa na kibwagizo kisichobadilika. Katika hali kama hii, maneno yote yaliyomo katika kibwagizo hurudiwa katika beti zote za shairi. Kurudiwa kwa kibwagizo ni kurudiwa kwa dhamira kwa lengo la kutilia mkazo. Siyo mashairi yote ya Shaaban Robert ambayo yana kibwagizo, lakini yale yaliyo nacho, uamilifu wake ni kama ulivyoelezwa katika sehemu hii. Mfano wa shairi lililo na kibwagizo ni lile la “Hofu” ambalo limerejelewa hapo juu. Mfano maarufu zaidi ni ule wa shairi la “Kiswahili” katika diwani ya *Pambo la Lugha* (uk. 27-31) ambapo mstari ule ule umerudiwa mwishoni mwa beti zote 31. Kibwagizo hicho ni: “Titi la mama litamu, jingine halishi tamu”. Hii ni sitiari inayolinganisha lugha ya kwanza, hususani Kiswahili, na titi la mama. Inaleta msisitizo mkubwa kwenye mtu kuipenda, kuithamini na kuifurahia lugha yake. Huu ni utetezi na uoneaji fahari Kiswahili ambao hauna kifani.

Nahau

Mfano wa kwanza wa matumizi ya nahau unapatikana katika diwani ya *Sanaa ya Ushairi*, shairi lenye kichwa: “Swali langu ni ujane” (uk. 44-47). Ubeti wa sita unasema:

Mpaka sasa nakaza, ujane ima fa ima,
Si neno la kupendeza, masikini la heshima,
Ni kitu kinapoteza, chastahili kukoma,
Swali langu ni ujane, si namna ya kuoa.

Nahau inayohusika imepigwiwa mstari. Hii ni nahau yenye asili ya Kiarabu ambayo imeundwa kwa kurudia neno “ima”, ambalo katika lugha hiyo lina maana ya “simama”. Tukumbuke kwamba nahau ni aina ya fumbo ambalo maana yake haitokani moja kwa moja na maneno yanayoiunda. Maana ya nahau hii katika matumizi ya kawaida ni kwa vyovyote vile. Katika muktadha wa ubeti wa hapo juu, nahau hii imetumiwa kukanusha kwa nguvu kwamba ujane una manufaa yoyote. Ukanushaji huu unaendelezwa katika mistari inayofuata. Fasiri hii ya nahau tunayoizungumzia ni kama muhtasari wa dhamira ya shairi zima ambayo inahusu kupinga ujane huku madhara yake yakibainishwa. Hapa tunaona jinsi nahau fupi ya maneno matatu inavyoweza kutoa mwanga juu ya wazo kuu linalotawala utungo mzima.

Inafaa kugusia mbinu nyingine inayoelezeka kama aina ya uchipuzi wa kileksika, hata kama haihusiani na nahau kwa njia ya moja kwa moja. Mbinu hiyo inahusu matumizi ya neno la tatu katika mstari wa kwanza: “nakaza”. Mbinu inayohusika hapa ni inkisari, ambapo neno la kawaida “nakazia” limefupishwa kwa ajili ya kupata idadi ya mizani ifaayo, na pia kina cha ukwapi, **-za**. Kukazia ni kushikilia jambo. Kwa hivyo, hili ni neno muafaka la kutilia mkazo msimamo wa msemaji juu ya suala la ujane. Katika diwani ya *Almasi za Afrika*, shairi la “Konde” (uk. 41), tunapata mfano mwingine wa matumizi ya nahau. Katika ubeti wa kwanza tunasoma ifuatavyo:

Konde mkulima konde, uso haukutakata,
Nalima katika bonde, makusudi ya kupata,
Mbona unaniweka shonde, pasipo kuteta vita?

....

Mbinu ya ritifaa ambapo msemaji anamuongelesha mtu asiyekuwapo kama kwamba anakabiliiana naye uso kwa uso imetumiwa kwa ufanifu mkubwa kuwasilisha hisia ya mapenzi. Nahau inayohusika imepigwiwa mstari. Kama tunavyojua, nahau huwa na muundo funge kwa

maana ya kwamba mtumiaji hana uhuru wa kuifanyia mabadiliko yoyote. Yaani, hawezi kubadilisha miundo ya maneno au mpangilio wake. Kwa mfano, katika sentensi inayotumia nahau kama “Maria amekuwa mwalimu wa uchochezi siku hizi”, nahau hii haiwezi kubadilishwa ikawa, “Maria amekuwa mkufunzi wa uchochezi siku hizi.” Katika sehemu ya shairi iliyonukuliwa hapo juu, nahau inayohusika ni “wekea shonde” ambayo ina maana ya kumnyamazia mtu kwa sababu ya kukasirishwa naye. Mtunzi ametumia idhini ya kishairi – kupitia mbinu ya inkisari – akalifupisha neno la kwanza la nahau hiyo. Sababu ni kupata idadi ya mizani inayofaa. Hata hivyo, hili ni badiliko dogo ambalo halimtatizi msomaji katika kuitambulisha na kuifasiri nahau inayohusika ipasavyo. Katika shairi linalozungumziwa, matumizi ya nahau iliyotajwa ni muhimu katika uendelezaji wa maudhui ambayo kiini chake ni malalamiko ya msemaji kwa mpenziwe anayerejelewa kisitiari kama konde. Msemaji huyo anaona uchungu kununiwa na mpenzi wake bila sababu iliyo wazi. Jitihada za kumfurahisha ambazo zinamithilishwa na kazi ya mkulima kondeni zinaambulia patupu.

Hitimisho

Makala hii imeshughulikia uchipuzi wa kileksika katika mashairi ya Shaaban Robert kwa lengo la kuonesha kwamba kwanza, kuna aina nyingi za uchipuzi wa aina hii, na pili, kila unapotokea unatoa mchango muhimu katika ujumbe na maudhui ya shairi kwa jumla. Tumeona kwamba baadhi ya mbinu ambazo mshairi ametumia kuzua uchipuzi ni urudiaji ambao unahusisha matumizi ya anafora, epanalepsia na kibwagizo. Mbinu nyingine ni maneno ya kizamani, nahau na rejesta mbalimbali. Mifano hii ya kutumia maneno kwa njia isiyo ya kawaida zinamvutia msomaji kiasi kwamba anataka kujua sababu za kuvunjwa kwa kaida na kanuni za lugha zinazohusika. Udadisi huu unapelekea kwenye fasiri ambayo, kama tulivyoona hapo juu, inadhihirisha mchango muhimu wa uchipuzi katika ujumbe wa shairi zima. Kwa hivyo, hatimaye uchipuzi unakuwa moja katika mikakati mikuu ambayo mshairi anatumia kuwasilisha ujumbe wake.

Uchipuzi hujitokeza katika viwango mbalimbali vya matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Licha ya kiwango cha maneno, unajitokeza pia katika viwango vya sarufi, uakifishaji,

sintaksia na semantiki. Matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbiha, sitiari, kwelikinanzi/paradoksi, chuku, tashihisi, n.k. yanachukuliwa kama ukengeukaji wa kisemantiki. Hii ni aina nyingine muhimu ya uchipuzi. Wachunguzi wa baadaye wanaweza kushughulikia viwango hivyo vya uchipuzi katika mashairi ya Shaaban Robert. Mashairi hayo yana ukwasi mkubwa wa sifa hiyo katika viwango vyote vilivyotajwa.

Marejeleo

- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri*. Kenya Literature Bureau.
- Baldick, C. (2008). *The oxford dictionary of literary terms*. Oxford University Press.
- Crystal, D. na Davy, D. (1969). *Investigating English style*. Longman.
- Enkvist, N.E. (1964). *Linguistics and style*. Oxford University Press.
- Gibbe, A.G. (1980). *Shaaban Robert: Mshairi*. Tanzania Publishing House.
- Hough, G.C. (1969). *Style and stylistics*. Routledge & Kegan Paul.
- Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. East African Literature Bureau.
- Leech, G.N. (1969). *A linguistic guide to English poetry*. Longman.
- Leech, G.N. na Short, M. (1981). *Style in fiction*. Longman.
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. TUKI.
- Mbatiah, M. (2008). “Shaaban Robert as a champion of peace” katika Indangasi, H. na Hashimoto, M.O. (Wah.). *Daisaku Ikeda and voices of peace from Africa* (uk. 57-64). Kenya Literature Bureau.
- _____ (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Mwansoko, H. J. M. (1991) *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam University Press.
- Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African novel*. Heinemann Educational Books.
- Robert, S. (1953). *Pambo la lugha*. Witwatersrand University Press.
- _____ (1966). *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini*. Thomas Nelson.
- _____ (1967 a). *Utenzi wa vita vya uhuru: 1939 hata 1945*. Oxford University Press.
- _____ (1967 b). *Masomo yenye adili*. Thomas Nelson.

- _____ (1967 c). *Insha na mashairi*. Thomas Nelson.
- _____ (1968 a). *Ashiki kitabu hiki*. Thomas Nelson.
- _____ (1968 b). *Mashairi ya Shaaban Robert*. Evans Brothers.
- _____ (1968 c). *Kielezo cha fasili*. Thomas Nelson.
- _____ (1969 a). *Koja la lugha*. Oxford University Press.
- _____ (1969 b). *Mwafrika aimba*. Thomas Nelson.
- _____ (1970). *Mapenzi bora*. Evans Brothers.
- _____ (1972 a). *Sanaa ya ushairi*. Thomas Nelson.
- _____ (1972 b). *Almasi za Afrika*. Thomas Nelson.
- Simpson, P. (2004). *Stylistics*. Routledge.
- Verdonk, P. (2003). *Stylistics*. Oxford University Press.
- Wales, K. (1989). *A Dictionary of stylistics*. Longman.
- Wellek, R. na Warren, A. (1985). *Theory of literature*. Penguin Books.

Kiambatisho

Tafsiri za istilahi muhimu

Anafora/mrejeosabiki – anaphora	Kuchanganya msimbo – code mixing
Chuku – hyperbole	Kweli-kinzani/paradoksi – paradox
Dhamira – theme	Leksisi – lexis
Diwani – anthology	Lughateule – diction
Elimumitindo – stylistics	Lugha ya kwanza – first language
Fahiwa – sense	Maadili – morals
Fasiri – interpretation	Maneno ambajengo – constituent words
Idhini ya kishairi – poetic license	Maneno ya kizamani – archaisms
Istilahi – terminology	Matini – text
Kaida – convention	Mbinu – device
Kanuni – rule/principle	Mbolezi – elegy
Kategoria za maneno – parts of speech	Msemaji – speaker
Kiambishi – affix	Msisitizo – emphasis
Kibwagizo/kituo – refrain	Mtaala (nomino) – study
Kinyambuo – derivative	Mtindo – style
Kipashio – unit	Mzizi – root
	Nahau – idiom

Neno mkopo – loan word	Uakifishaji – punctuation
Pasona – persona	Uamilifu – function
Rejesta – register	Uchipuzi – foregrounding
Ridhimu/wizani – rhythm	Uchipuzi wa kileksika – lexical foregrounding
Ritifaa - apostrophe	Uhakiki wa kifasihi – literary criticism
Ruwaza – pattern	Ujumbe – message
Sitiari – metaphor	Ukengeukaji/ukiushi – deviation
Tajiriba – experience	Ukopaji – borrowing
Talii – study	Ukwapi – first hemistich
Tamathali za usemi – figures of speech	Unyambulishaji – derivation
Tasfida – euphemism	Urudiaji – repetition
Tashbiha – simile	
Tashihisi – personification	